# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***10 Agosti, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongoza Watanzania kuaga mwili wa Mbunge wa Kongwa na Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Job Yustino Ndugai, leo katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.

Rais Dkt. Samia ametoa salamu za pole kwa Watanzania, wana-Kongwa, Bunge, Kanisa la Anglikana na Chama cha Mapinduzi kufuatia msiba huo, akimtaja Hayati Ndugai kama kiongozi shupavu aliyeacha alama isiyofutika katika historia ya Taifa.

***"Tumepoteza nguzo muhimu ya Taifa, Kiongozi aliyeaminiwa ndani na nje ya nchi, aliyejituma bila kuchoka katika kutumikia wananchi na kulinda maslahi ya Taifa,"*** alisema Rais. Dkt. Samia.

Rais Dkt. Samia amesema Hayati Ndugai atakumbukwa kwa kuongoza mageuzi muhimu ndani ya Mhimili wa Bunge, yakiwemo kuliingiza Bunge kwenye mfumo wa kidijitali kupitia 'Bunge Mtandao' na kuanzisha Kamati Maalum nne za ushauri kwa Serikali kuhusu rasilimali za Taifa kama almasi, tanzanite, gesi na uvuvi wa bahari kuu, hatua zilizoimariha usimamizi wa rasilimali na kuongeza mchango wake kwenye pato la Taifa.

Aidha, amemtaja Ndugai kama kiongozi aliyejali maendeleo ya vijana na elimu, akihamasisha ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge na kusaidia vijana wengi kufikia elimu ya juu.

Rais Dkt. Samia pia ameeleza jitihada za Hayati Ndugai katika kuleta maendeleo ya miundombinu ya elimu, afya na umeme akiwa Mbunge wa Jimbo la Kongwa alilohudumu tangu mwaka 2000 alipochaguliwa kwa mara ya kwanza.

Rais Dkt. Samia amehitimisha kwa kusema Serikali itaendelea kuenzi mchango mkubwa alioutoa Hayati Job Yustino Ndugai kwa Taifa katika nyanja mbalimbali.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu